



Mtakatifu Josemaria Escriva

Mwanzilishi wa Opus Dei

SALA

Ee Mungu, kwa maombezi ya Bikira Maria, ulimjalilia padri wako Mtakatifu Josemaria neema nyingi, ukamchagua kuwa mtume wako mwaminifu ili aanzishe Opus Dei, njia ya kujitakasa katika kazi ya kila siku na katika kutimiza wajibu wa kawaida wa Mkristu. Nisaidie mimi pia ili nami niweze kuyafanya mambo yote ya maisha yangu yawe nafasi ya kukupenda na kulitumikia Kanisa, Baba Mtakatifu na watu wote, kwa furaha na moyo mwepesi, nikiangaza njia zote duniani kwa mwanga wa imani na upendo. Kwa maombezi yake Mtakatifu Josemaria, nijalie msaada ninaokuomba... (taja ombi lako hapa). Amina.

Baba yetu, Salamu Maria, Atukuzwe Baba.

Popote pale ilipo kazi yako, yalipo matakwa yako, mapenzi yako; hapo ndipo pahali pako hasa pa kukutana na Kristu kila siku. Ni katika mambo ya kawaida, ya ulimwengu, ambapo inatupasa kujitakasa, tukimtumikia Mungu na watu wote. Wanangu, kwenye upeo wa macho huonekana kama kwamba mbingu na ardhi huungana. Walakini pale hasa zinapoungana ni mioyoni mwenu, mnapoyatakasa maisha yenu ya kila siku.

Mahubiri ya Mtakatifu Josemaria Escriva, kuhusu kuupenda ulimwengu kwa dhati, aliyoyatoa Oktoba 8, 1967.

Mtakatifu Josemaria Escriva alizaliwa mjini Barbastro, Uhispania, mnamo tarehe 9 Januari, 1902. Alipata sakramenti ya upadri tarehe 28 Machi, 1925 mjini Saragosa. Kwa mwongozo wa Mungu, tarehe 2 Oktoba 1928, aliianzisha Opus Dei. Tarehe 26 Juni 1975, alikufa ghafla mjini Roma chumbani mle alimozoea kufanyia kazi yake, baada ya kuitupia jicho la upendo picha ya mama yetu, Maria. Kufikia hapo, Opus Dei ilikuwa imekwisha kusambaa katika mabara yote matano ya ulimwengu, ikiwa na wanachama zaidi ya 60,000 kutoka mataifa 80, wanaoliumikia kanisa kwa moyo mmoja, wakijiuga kikamilifu na Baba Mtakatifu pamoja na Maaskofu, kama ilivyokuwa desturi yake Mtakatifu Josemaria. Baba Mtakatifu John Paul II alimfanya mwanzilishi wa Opus Dei kuwa Mtakatifu tarehe 6 Oktoba 2002 mjini Roma. Sikukuu yake inasherehekewa tarehe 26 Juni. Mwili wa Mtakatifu Josemaria umelazwa katika kanisa kuu la Prelature ya Opus Dei liitwalo 'Mama Yetu wa Amani', katika barabara ya Bruno Buozzi 75, mjini Roma.

Maelezo zaidi kuhusu Mtakatifu Josemaria Escriva yanaweza kupatikana, kwenye mtandao wa www.opusdei.org na www.josemariaescriva.info

Wanaojaliwa misaada kupitia kwa maombezi ya Mtakatifu Josemaria Escriva wanaombwa kuiarifu Prelature ya Opus Dei kupitia, ofisi ya Uchunguzi wa Watakatifu, Sanduku la Posta, 49569, 00100 GPO Nairobi, Kenya.

Imeidhinishwa na Kanisa.